*GN. No. 443*

In the matter of an Application by the

**SIKONGE WATER SUPPLY AND SANITATION AUTHORITY (SIKONGE WSSA)**

For a multi-year tariff adjustment

Background

1. On 13th May 2018, the Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA) received Tariff Application from Sikonge Water Supply and Sanitation Authority (Sikonge WSSA) for a multi-year tariff and charges review for water supply covering a period from 2018/19 to 2020/21. Sikonge WSSA requested:

a) to increase metered water tariffs at a range between 64% and 400% in 2018/19; 3% and 4% in 2019/20 and an increase of 3% in 2020/21;
b) to introduce service charges of TZS. 1000/month for all customer categories except for watering animal which its charge is proposed to be TZS 2,500/month;
c) to increase water connection fee in the range between 33% and 67% in 2018/19 and maintain the same for 2019/20 and 2020/21;
d) to increase water reconnection fees by 163% in 2018/19 and no change in 2019/20 and 2020/21;
e) to increase meter rent by 150% in 2018/19 and no further increase in 2019/20 and 2020/21; and
f) to introduce water connection application form fee

of TZS 5000/form for all customer categories except kiosk and bowser customer categories.

Tariff Review Justification

2. The main justification for tariff review given by Sikonge WSSA is due to insufficient revenue caused by current tariffs that do not meet the actual costs of operation and maintenance. According to Sikonge WSSA, the benefits to the customers which will be obtained if the proposed tariff and charges are approved include: attain full cost recovery and hence among other things improve water quality, ensure utility's sustainability and satisfy customers' needs.

Stakeholders' Consultation

3. Pursuant to Section 19(2)(b) of the Energy and Water Utilities Regulatory Authority Act, Cap. 414, EWURA conducted an Inquiry into the reasonableness of the proposed adjustments for tariff and charges. This Inquiry included an economic, technical evaluation of the Application and a Public hearing meeting that was held in Sikonge Town on 14th June 2018 to collect views from the stakeholders.

GCC was concerned, among other things, about lack of audited financial statements, low proposed service hours from the current 10 hours to 12 hours by 2020/21, low proposed tariffs for the second and third year compared with the significant proposed tariff in the first year and unattained key performance indicators as stated in the business plan.

EWURA CCC was concerned, among other things, about non adherence to the Tariff Setting Guidelines of 2017, proposed expansion of water network is very small, very low targets for proposed key performance indicators and lack of evidence/study on affordability

The Public was concerned, among other things, about

significant proposed increase of tariff in the first year, high proposed reconnection charges, limited water distribution network and unspoken issues on sanitation services

At the closure of the Inquiry process on 20th June 2018, EWURA had gathered adequate information to prudently determine the application.

Analysis and Adjustment

4. As a result of the Inquiry and evaluation process, EWURA concluded that the proposed increase in multi-year tariff and charges by Sikonge WSSA were reasonable except for some operation and maintenance costs that were on a high side and lack justifications. Based on that, EWURA decided to allow a Revenue Requirement (RR) of TZS 519.12 million for the review period (2018/19 – 2020/21) which is equivalent to 72% of TZS 721.61 million as RR proposed by Sikonge WSSA.

The adjusted Operation and Maintenance Costs (O& M) and Revenue Requirement (RR) for Sikonge WSSA during the period from 2018/19 to 2020/21 are as shown in Tables 1and 2

**Table 1: Adjusted O & M Costs (Million TZS)**

| COST | 2018/19 | | 2019/20 | | 2020/21 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Proposed | Adjusted | Proposed | Adjusted | Proposed | Adjusted |
| Water production | 22.49 | 8.02 | 23.16 | 10.45 | 23.86 | 12.53 |
| Diesel for water production | 48.75 | 73.79 | 50.21 | 96.85 | 51.72 | 122.03 |
| Water Distribution | 35.90 | 0.00 | 36.97 | 0.20 | 38.08 | 0.00 |
| Maintenance and Repair | 7.00 | 1.91 | 7.21 | 2.01 | 7.43 | 2.11 |
| Personnel | 60.61 | 35.66 | 62.43 | 37.36 | 64.30 | 39.14 |
| Administrati | 31.17 | 14.08 | 32.11 | 14.76 | 33.07 | 15.48 |
| Business promotion | 5.90 | 0.84 | 6.07 | 0.88 | 6.26 | 0.93 |
| Events and Donation | 10.95 | 0.26 | 11.28 | 0.28 | 11.62 | 0.29 |
| Board | 15.00 | 3.57 | 15.45 | 3.58 | 15.91 | 3.59 |
| Finance | 0.70 | 0.00 | 0.72 | 0.00 | 0.74 | 0.00 |
| **TOTAL** | **238.4** | **138.1** | **245.6** | **166.3** | **252.99** | **196.0** |

**Table 2: Adjusted RR (Million TZS)**

| Description | 2018/19 | | 2019/20 | | 2020/21 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Proposed | Adjusted | Proposed | Adjusted | Proposed | Adjusted |
| Operating and Maintenance | 238.47 | 138.13 | 245.62 | 166.36 | 252.99 | 196.09 |
| Depreciation allowance | 5.68 | 0 | 6.24 | 0 | 6.87 | 0 |
| Allowed Investment | 0 | 7.75 | 0 | 9.24 | 0 | 9.35 |
| **Total Revenue Requirement** | **244.15** | **145.88** | **251.86** | **175.6** | **259.86** | **205.44** |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Less Other Income | (10.33) | (2.48) | (11.36) | (2.60) | (12.50) | (2.73) |
| **RR from water sales** | **233.81** | **143.4** | **240.50** | **173.00** | **247.36** | **202.72** |

| | |
|---|---|
| Decision | 5. The Board of Directors of EWURA having met on 27th July 2018 to consider this matter decided as per the Order below: |

THE WATER SUPPLY AND SANITATION ACT
(CAP. 272)
*(Made under section 28(d))*

**THE SIKONGE WATER SUPPLY AND SANITATION AUTHORITY ("SIKONGE WSSA") TARIFF ADJUSTMENT ORDER, 2018**

Citation

1. This Order shall be cited as the Sikonge Water Supply and Sanitation Authority ("Sikonge WSSA") (Tariff Adjustment for Water Supply and Sanitation Services) Order, 2018.

Commencement Date

2. This Order shall come into force on 1st September 2018.

Tariffs and Charges

3. Sikonge WSSA tariffs and charges are hereby adjusted as specified in the First Schedule to this Order.

Conditions

4. The approved tariff shall be subject to the following conditions:

a) On or before 31st December 2018, Sikonge WSSA shall submit a revised Business Plan

that incorporates the approved tariffs and action plan for implementation of conditions of this Order.

b) Sikonge WSSA shall implement the projects as detailed in Second Schedule by using funds generated from the approved tariffs.

c) Sikonge WSSA shall attain the key performance indicators as shown in the Third Schedule of this Order.

d) Sikonge WSSA shall cause their financial reports to be audited by a CAG or any authorized person as per section 33 (1) of the Public Audit Act and ensure that it submits copies of the audited financial statements to EWURA.

e) On or before 30$^{th}$ June 2019, Sikonge WSSA shall undertake valuation of their assets and submit to EWURA an Asset Valuation Report certified by a registered Valuer.

f) Sikonge WSSA shall, on annual basis as part of its annual perfomance report, submit to EWURA reports on the implementation of each of the Tariff Order condition and each cost item of the revenue requirement.

g) Sikonge WSSA shall continue to provide EWURA with information about its financial and operating condition in accordance

with the requirements of EWURA. This information will be used by EWURA to evaluate Sikonge WSSA's performance in comparison with other Water Supply and Sanitation Authorities and the improvement of its performance over time. This evaluation will be considered by EWURA in evaluating the reasonableness of all future requests for tariff adjustment.

Disapplication of Tariff Order No. 11-014 of 1st June 2011

This Order hereby disapplies the applicability of the (Tariff Adjustment) Order No. 11 - 014 of 1st June 2011 in the area served by the Sikonge Water Supply and Sanitation Authority (Sikonge WSSA).

*GN. No. 443*

## SCHEDULES

### FIRST SCHEDULE: APPROVED TARIFFS AND CHARGES

**Schedule 1(a): Current and Approved Water Tariff (TZS/$m^3$)**

| Customer Category | Current Tariff | Approved Tariff | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Domestic | 800 | 1,350 | 1,390 | 1,470 |
| Commercial | 935 | 1,575 | 1,625 | 1,715 |
| Institution | 900 | 1,515 | 1,565 | 1,650 |
| Industrial | | 1,595 | 1,645 | 1,735 |
| Kiosk | 1,000 | 1,500 | 1,500 | 1,500 |
| **WAT** | **844.43** | **1,416** | **1,458** | **1,536** |

**Schedule 1(b): Current and Approved Multi-Year Service Charge (TZS/Month)**

| Customer Category | Current Charges | Approved Charges | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Domestic | 0 | Not approved | | |
| Commercial | 0 | | | |
| Institution | 0 | | | |
| Industrial | 0 | | | |

**Schedule 1 (c): Current and Approved Multi-Year Water Connection Fee (TZS/Connection)**

| Customer Category | Current Fee | Approved Fees | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Domestic | 15,000 | 20% of recoverable expenditure as stipulated in Section 24 of Water Supply Regulation, 2013 | | |
| Commercial | 15,000 | | | |
| Institution | 15,000 | | | |
| Industrial | 15,000 | | | |

**Schedule 1 (d): Current and Approved Water Reconnection Fee (TZS/Reconnection)**

| Customer Category | Current Fee | Approved Fees | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Domestic | 4,000 | 10,500 | 10,500 | 10,500 |
| Commercial | 4,000 | 10,500 | 10,500 | 10,500 |
| Institution | 4,000 | 10,500 | 10,500 | 10,500 |
| Industrial | NA | 24,300 | 24,300 | 24,300 |

*GN. No. 443*

**Schedule 1(e): Current and Approved Meter Rent (TZS/Month)**

| Customer Category | Current Rents | Recommended Rents | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Domestic | 800 | Not Allowed | | |
| Commercial | 800 | | | |
| Institution | 800 | | | |
| Industrial | NA | | | |

**Schedule 1(f):Current and Approved Water Connection Application Form Fees - TZS/Form**

| Customer Category | Current Fee | Approved Fees | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Domestic | 0 | Not Approved | | |
| Commercial | 0 | | | |
| Institution | 0 | | | |
| Industrial | 0 | | | |

**SECOND SCHEDULE**

**PROJECTS TO BE IMPLEMENTED**

| Description of the Activity | TZS | | | Deadline |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | |
| **Replacement of Asetts** | | | | |
| Purchase 12 class C DN 20mm water meters each year for replacement of defects meters | 1,134,000 | 1,190,700 | 1,250,235 | June of each year |
| **Subtotal (Replacement )** | **1,134,000** | **1,190,700** | **1,250,235** | |
| **New Investments** | | | | |
| Purchase 70 class C DN 20mm water meters each year for new customers. | 6,615,000 | 6,945,750 | 7,293,038 | June of each year |
| Purchase of one sluice valve of DN 80mm in 2019/20, one sluice valve of DN 100mm in 2020/21 and their respective connection fittings. | | 1,102,500 | 810,338 | June 2020 and June 2021 |
| **Subtotal - (New Investments)** | **6,615,000** | **8,048,250** | **8,103,375** | |
| **Total Investment Cost** | **7,749,000** | **9,238,950** | **9,353,610** | |

**THIRD SCHEDULE**

**KEY PERFORMANCE INDICATORS FOR 2018/19 – 2020/21**

| Description | Unit | Perfomance Target | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| New Connections (water) | No. | 70 | 70 | 70 |
| Non Revenue Water | % | 23 | 21 | 20 |
| Metering Ratio | % | 100 | 100 | 100 |
| Revenue Collection efficiency (without arrears) | % | 87 | 88 | 90 |

**Dar es Salaam**
**27th July 2018**

**Nzinyangwa E. Mchany**
**Director General**

*GN. No. 443*

Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified

Ombi la Kurekebisha Bei za Majisafi na Usafi wa Mazingira la

**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA SIKONGE (SIKONGE WSSA)**

Utangulizi

**1.** Mnamo tarehe 13 Mei 2018, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ("EWURA") ilipokea ombi kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sikonge (Sikonge WSSA) kwa ajili ya marekebisho ya bei za majisafi kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2020/21 kwa ajili ya mapitio na maidhinisho. Sikonge WSSA iliomba:

a) kuongeza bei kwa wateja wa maji kwa kiwango cha kati ya asilimia 64 na asilimia kwa mwaka 2018/19, asilimia 3 na asilimia 4 kwa mwaka 2019/20 na ongezeko la asilimia 3 kwa mwaka 2020/21;
b) kuanzisha tozo ya huduma ya shilingi 1000/mwezi kwa wateja wote isipokuwa kwa wateja wa maji kwa ajili ya kunyweshea mifugo ambayo tozo inayopendekezwani shilingi 2,500/mwezi ;
c) kuongeza ada ya maunganisho mapya ya maji kwa ongezeko la kati ya asilimia 33 na 67 kwa mwaka 2018/19 na kuendelea kwa ada hizo kwa mwaka 2019/20 na 2020/21;
d) kuongeza ada ya kurejeshewa huduma ya maji kwa ongezeko la asilimia 163% na kuendelea kutumia ada hizo kwa mwaka 2019/20 na 2020/21;
e) kuongeza kodi ya dira kwa asilimia 150 kwa mwaka 2018/19 na hakuna ongezeko kwa mwaka 2019/20 na 2020/21; na
f) kuanzisha ada ya fomu kwa wateja wanaoomba kuunganishwa katika huduma za maji ya shilingi 5000/fomu kwa wateja wote isipokuwa wateja wa magati na boza.

Sababu za Kurekebisha Bei

**2.** Sababu zilizotolewa na Sikonge WSSA kuhusu mapendekezo ya bei na tozo ni kutokana na kutokuwa na mapato yasiyojitosheleza yanayosababishwa na bei ambazo hazikidhi gharama za uendeshaji na matengenezo. Sikonge WSSA imeeleza kuwa iwapo bei na ada zilizopendekezwa zitaidhinishwa faida watakazopata wateja ni pamoja na:

kurudisha gharama zote za huduma ili pamoja na mambo mengine, kuhakikisha uendelevu wa Sikonge WSSA na kuridhisha mahitaji ya wadau.

Ushirikishwaji wa Wadau

**3.** Kwa mujibu wa kifungu cha 19(2)(b) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414, EWURA ilifanya taftishi kuhusu uhalali wa ombi la kurekebisha bei zilizopendekezwa. Taftishi hiyo ilihusisha tathmini ya masuala ya kiuchumi na ya kiufundi pamoja na kukusanya maoni kutoka kwa wadau katika mkutano uliofanyika katika mji wa Sikonge mnamo tarehe 14 Juni 2018.

GCC walihoji, pamoja na mambo mengine, kuhusu kukosekana kwa taarifa za fedha zilizokaguliwa, masaa machache ya huduma yaliyopendekezwa kutoka masaa 10 ya sasa mpaka masaa 12 ifikapo mwaka 2020/21, na pendekezo la bei dogo kwa mwaka wa pili na wa tatu ukilinganisha na pendekezo kubwa la bei kwa mwaka wa kwanza.

EWURA CCC walihoji, pamoja na mambo mengine, kuhusu kutokuzingatiwa kwa Mwongozao wa Upangaji Bei wa Mwaka 2017, mapendekezo madogo ya kuongeza mtandao wa maji, na malengo ya chini sana ya viashiria vya kiutendaji.

Wananchi walihoji, pamoja na mambo mengine, kuhusu mapendkezo makubwa ya bei za maji kwa mwaka wa kwanza, mapendekezo makubwa ya gharama za kurejeshewa huduma, mtandao wa maji mdogo na kutoongelewa kwa masuala ya usafi wa mazingira.

Hadi wakati wa kuhitimisha taftishi mnamo tarehe 20 Juni 2018, EWURA ilikuwa imepokea maoni ya kutosha kuweza kufanya maamuzi juu ya ombi la Sikonge WSSA la kurekebisha bei za majisafi.

Uchambuzi na Marekebisho

**4.** Kufuatia kukamilika kwa mchakato wa taftishi na uchambuzi, EWURA imefikia uamuzi kwamba ombi la marekebisho ya bei na tozo la Sikonge WSSA lina mantiki na ni halali isipokuwa kwa baadhi ya gharama za uendeshaji na matengenezo na miradi zilizopendekezwa kuwa kubwa bila sababu na kukosa uhalali. Kutokana na hayo, EWURA imeamua kuruhusu Mahitaji ya Mapato kwa kiasi cha shilingi 519.12 milioni kwa kipindi cha 2018/19 – 2020/21 ambayo ni sawa na asilimia 72 ya fedha zilizoombwa na Sikonge WSSA.

Uamuzi

**5.** Katika kikao chake cha tarehe 27 Julai 2018, Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA ilijadili ombi hili na kutoa maamuzi kama inavyooneshwa kwenye Agizo hapo chini:

*GN. No. 443*

**SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA**
**(SURA NA 272)**

*(Imetolewa kwa mujibu wa Kifungu Na.28 (d))*

**AGIZO LA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA SIKONGE ("SIKONGE WSSA"), LA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA), 2018**

Kichwa cha Agizo

**1.** Agizo hili litajulikana kama, Agizo la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sikonge ("Sikonge WSSA"), (la Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira), la Mwaka 2018.

Tarehe ya Kuanza

**2.** Agizo hili litaanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Septemba 2018.

Marekebisho ya Bei

**3.** Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Sikonge WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Agizo hili.

Masharti

**4.** Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) Ifikapo tarehe 31 December 2018 au kabla, Sikonge WSSA itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Agizo hili.

(b) Sikonge WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Agizo hili.

(c) Sikonge WSSA itafikia viashiria vya

utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Agizo hili.

(d) Sikonge WSSA itahakikisha kuwa taarifa zake za fedha zinakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) au mtu yeyote aliyeidhinishwa kutokana na kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma na kuhakikisha inawasilisha EWURA rasimu za mahesabu yaliyokaguliwa.

(e) Ifikapo tarehe 30 Juni 2019 au kabla, Sikonge WSSA itafanya tathmini ya thamani ya mali zake na kuwasilisha EWURA taarifa ya tathmini iliyothibitishwa na Mtathmini aliyesajiliwa.

(f) Sikonge WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Agizo la Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa.

(g) Sikonge WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Sikonge WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa

huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Sikonge WSSA katika siku zijazo.

Agizo Na. 11-014 la tarehe 1 Juni 2011

Agizo hili linasitisha matumizi ya Agizo Na. 11-014 la tarehe 1 Juni 2011 katika maeneo yanayohudumiwa na Sikonge WSSA.

*GN. No. 443*

# MAJEDWALI

## JEDWALI LA KWANZA: BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

**Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ mita ya ujazo)**

| Kundi la Wateja | Bei za Sasa | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 800 | 1,350 | 1,390 | 1,470 |
| Biashara | 935 | 1,575 | 1,625 | 1,715 |
| Taasisi | 900 | 1,515 | 1,565 | 1,650 |
| Viwanda | | 1,595 | 1,645 | 1,735 |
| Magati | 1,000 | 1,500 | 1,500 | 1,500 |
| **Wastani wa Ulinganisho** | **844.43** | **1,416** | **1,458** | **1,536** |

**Jedwali Namba 1(b): Tozo ya Huduma ya Sasa na Iliyoidhinishwa (Shilingi/Mwezi)**

| Kundi la Wateja | Tozo ya Sasa | Tozo Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 0 | Tozo ya Huduma haijaidhinishwa | | |
| Biashara | 0 | | | |
| Taasisi | 0 | | | |
| Viwanda | 0 | | | |

**Jedwali Namba 1(c): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho ya Maji Safi (Shilingi/Maunganisho)**

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |

| **Kundi la Wateja** | **Ada ya Sasa** | **Ada Iliyoidhinishwa** | | |
|---|---|---|---|---|
| | **2017/18** | **2018/19** | **2019/20** | **2020/21** |
| Majumbani | 15,000 | Asilimia ishirini ya gharama za maunganisho kama inavyojieleza katika sehemu ya 24 ya Kanuni za Maji za mwaka 2013 | | |
| Biashara | 15,000 | | | |
| Taasisi | 15,000 | | | |
| Viwanda | 15,000 | | | |

**Jedwali Namba 1(d): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)**

| **Kundi la Wateja** | **Ada ya Sasa** | **Ada Iliyoidhinishwa** | | |
|---|---|---|---|---|
| | **2017/18** | **2018/19** | **2019/20** | **2020/21** |
| Majumbani | 4,000 | 10,500 | 10,500 | 10,500 |
| Biashara | 4,000 | 10,500 | 10,500 | 10,500 |
| Taasisi | 4,000 | 10,500 | 10,500 | 10,500 |
| Viwanda | NA | 24,300 | 24,300 | 24,300 |

**Jedwali Namba 1(e): Kodi ya sasa na Iliyoidhinishwa ya Dira ya Maji (Shilingi/ Mwezi)**

| **Kundi la Wateja** | **Kodi ya Sasa** | **Kodi Iliyoidhinishwa** | | |
|---|---|---|---|---|
| | **2017/18** | **2018/19** | **2019/20** | **2020/21** |
| Majumbani | 800 | Kodi ya Dira ya Maji Hairuhusiwi | | |
| Biashara | 800 | | | |
| Taasisi | 800 | | | |
| Viwanda | NA | | | |

*GN. No. 443*

**Jedwali Namba 1(f): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Fomu za Kuomba Kuunganishiwa Huduma ya Majisafi – Shilingi/Fomu**

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 0 | Ada ya Fomu Hajaidhinishwa | | |
| Biashara | 0 | | | |
| Taasisi | 0 | | | |
| Viwanda | 0 | | | |

*GN. No. 443*

## JEDWALI LA PILI
## MIRADI ITAKAYOTOKELEZWA

| Maelezo ya Kazi zitakazofanyika | Shilingi | | | Tarehe ya Mwisho ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | |
| **Kubadilisha Mali** | | | | |
| Kununua dira za wateja 12 za daraja C DN 20mm kila mwaka kwa ajili ya kubadili dira zenye matatizo. | 1,134,000 | 1,190,700 | 1,250,235 | Juni ya kila mwaka |
| **Jumla Ndogo ya Mabadilisho** | **1,134,000** | **1,190,700** | **1,250,235** | |
| **Miradi Mipya** | | | | |
| Kununua na Kufunga mita 70 kila mwaka za daraja C DN 20mm kwa ajili ya wateja wapya. | 6,615,000 | 6,945,750 | 7,293,038 | Juni ya kila mwaka |
| Kununua sluice valve moja ya DN 80mm mwaka 2019/20, sluice valve moja ya DN 100mm mwaka 2020/21 and viungio vyake husika | | 1,102,500 | 810,338 | Juni 2020 and Juni 2021 |
| **Jumla ndogo ya uwekezaji mpya** | **6,615,000** | **8,048,250** | **8,103,375** | |
| **Jumla kuu ya** | **7,749,** | **9,238,950** | **9,353,6** | |

| **Maelezo ya Kazi zitakazofanyika** | **Shilingi** | | | **Tarehe ya Mwisho ya Utekelezaji** |
|---|---|---|---|---|
| | **2018/19** | **2019/20** | **2020/21** | |
| **gharama za uwekezaji** | **000** | | **10** | |

## JEDWALI LA TATU
## VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2018/19 – 2020/21)

| **Maelezo** | **Uniti** | **Lengo la Utendaji** | | |
|---|---|---|---|---|
| | | **2018/19** | **2019/20** | **2020/21** |
| Idadi ya wateja wapya wa maji safi | Na | 70 | 70 | 70 |
| Kiwango cha upotevu wa maji | % | 23 | 21 | 20 |
| Wateja wenye Dira | % | 100 | 100 | 100 |
| Kiwango cha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato | % | 87 | 88 | 90 |

Dar es salaam
27 Julai 2018

NZINYANGWA E. MCHANY
*Mkurugenzi Mkuu*

*GN. No. 443*